

TANGAZO TANGAZO TANGAZO
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU
(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

MKOA WA MWANZA

Simu:- 028 – 2530002

FaxNo.: -028 – 2530199



Sanduku la Posta 200
MAGU.

19.12.2019

TANGAZO LA UZAJI WA VIWANJA HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU

Mkurugenzi mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya magu anapenda kuwatangazia wananchi wote na umma kwa ujumla kuwa halmashauri imepima viwanja kwa ajili ya matumizi ya viwanda, makazi, na makazi na biashara.

Viwanja vya makazi na makazi na biashara vinapatikana katika mji wa kisesa mwambao mwa barabara ya lami ya kisesa-usagara umbali wa kilometa moja toka round about ya kisesa na kilometa kumi na tano toka katikati ya jiji la mwanza. Viwanja vinafikika kwa urahisi na tayari miundombinu ya barabara na umeme ipo

Viwanja vya matumizi ya viwanda vinapatikana katika eneo la Ihushi kata ya Bujashi mwambao mwa barabara ya Kisesa-Kayenze. Viwanja hivi vipo katika mazingira mazuri kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda.

Bei ya viwanja hivyo ni kama ifuatavyo:-

Na	MATUMIZI	BEI KWA MITA MOJA YA MRABA
1	Makazi	4,500/=
2	Makazi na biashara	5,500/=
3	Viwanda vidogo	1,500/=
4	Viwanda vya kati na vikubwa	1,000/=

Bei hizi ni pamoja na maandalizi ya hati miliki.

Waombaji wa viwanja wanatakiwa kuchukua na kujaza fomu za maombi ya viwanja am bazo zitatolewa katika Ofisi ya Ardhi kuanzia tarehe 23/12/2019 kuanzia saa 1:30 Asubuhi hadi saa 9:30 Alasiri. Gharama ya fomu hizo ni Tshs 20,000/= ambazo hazitarejeshwa.

Mwombaji atatikiwa kuchagua kiwanja anachokipenda na kulipa nusu ya gharama ya malipo ya kiwanja hicho. Kiasi kinachosalia kitatakiwa kulipwa ndani ya siku 90 tokea tarehe ya malipo ya awali kufanyika. Kama malipo hayo hayatakamilishwa ndani ya siku hizo, kiwanja kitatolewa kwa mwombaji mwingine na hakuna fedha itayorejeshwa.

Mwombaji anatakiwa kurejesha nakala ya stakabadhi aliyofanyia malipo katika ofisi za Ardhi kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za ofisi vizuri.

Tangazo hili limetolewa na

Lutengano G. Mwalwiba
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU